REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 8th March, 2022

The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) in the Chair]

PRAYERS

MOTION

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF WATER, ENVIRONMENT AND NATURAL RESOURCES

Hon. Simon Kanyutu through Hon. Wilson Wakahiu: Thank you Mr. Speaker. I wish to move the following motion;

THAT, this House adopts the quarterly report and financial statements for the period ended 30th September, 2020 for department of Water, Environment and Natural Resources by the Sectoral Committee on Agriculture, Environment and Natural Resources dated 23rd February, 2022.

Mr. Speaker Sir, the committee comprising of the following Members as was reconstituted for the second time on 28th September, 2021:

1. Hon. Simon Kanyutu - Chairperson
2. Hon. Patricia Muthoni - Vice Chairperson
3. Hon. Robert Maina - Member
4. Hon. Mutahi Muritu - Member
5. Hon. Wilson Wakahiu - Member
6. Hon. Peter Thomi - Member
7. Hon. Lochimidi J. Esokon - Member

Mr. Speaker Sir, according to Standing Order 177, the committee is limited to its mandate as follows:-

(1) The deliberations of a select committee shall be confined to the mandate of the committee and any extension or limitation of that mandate as may be directed by the Assembly and, in the case of a select committee on a Bill, to the Bill committed to it and relevant amendments.

(2) In the exercise of its functions, a select committee may not consider any matter that is not contemplated within the mandate of the Assembly under the Constitution.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker, Sir, the Committee has scrutinized the quarterly report for the said financial year and the following were the observations. The following information was derived from the quarterly report and financial statements for the period ended 30th September, 2020 for the financial year 2020/2021. During the period under review, the department of Water, Environment and Natural Resources approved budget, expenditures, absorption rate in Table 1 and received foreign grants in table 2:- I know Members has these copies with them and you can see how the original budget was.

Mr. Speaker, on page 4, I know Members have the programs and it has been outlined as I have said. Those were the observations and how the government utilized the budget for the said financial year. On behalf of Agriculture and Natural resources Committee, I wish to extend gratefulness for the support they have accorded this committee. Secondly, I wish to acknowledge Members of Agriculture and Natural resources Committee for the continued commitment.

Lastly Mr. Speaker, and I know Hon. Members will support this is what we got from the Executive and how the department has performed. I beg the Honourable Members to support this report so that we can move on to find the other documents on the expenditure of the government in the said department. Mr. Speaker, I request Hon. Thomi to second the report.

(Hon. Peter Thomi seconded)

(Question proposed)

Speaker: Don't we have Members of that committee? Not only members, you all have the report and you can be able to see and do contributions.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Mheshimiwa Spika. Nasimama kuunga mkono ripoti ya Idara ya Maji, Mazingira na mali asili. Bwana Spika, nafikiri hii ni idara ambayo inagusa mwananchi. Idara ya Maji inafaa kuangaliwa sana hasa wakati huu tuko na kiangazi. Kabla niangalie yale ambayo yako hapa, niruhusu niongee kuhusu hii idara kwa sababu tuko na shida hasa katika wadi ambayo nawakilisha. Wananchi ambao wako kwenye hiyo wadi hawana maji.

Bwana Spika, kuna kampuni ya NAWASCO ambayo inafaa kupatia wananchi maji lakini hii kampuni imekuwa ni *cartels* wako hapo. Hata kama imeharirishwa kisiasa, yale mambo ambayo yanafanyiwa mwananchi mashinani ni ya kinyama. Niliona mwananchi akitumiwa bili ya 300 na akichelewa kulipa hiyo pesa mwezi ujao analetewa adhabu ya 1000. Ndio maana nasema hii kampuni iko na unyama na wale ambao wanaongoza hiyo kampuni wanafaa kuangaliwa vizuri kwa sababu hawana nia njema na wananchi ambao tunawakilisha.

Ni vizuri wananchi ambao wanachaguliwa na wananchi wawe na kikao cha dharura kwa sababu wananchi wanateseka. Watu wanaitishwa pesa ambazo hazipatikani. Sioni ni kwa njia ipi unapatiwa adhabu kubwa kuliko ile pesa ambayo unafaa kulipa. Hapa kuna shida na wasipo badilisha tutapelekana na hawa watu kwa sababu kuna shida ambayo tunafaa kuangalia kwa umakini. Nashukuru Kamati kwa kuweza kuangalia vile Idara imeweza kutumia pesa yake.

Mimi naona ni ripoti ya robo ya mwaka uishao tarehe 31 Septemba, ambayo ni ya kwanza. Yale mambo ninayoyaona hapa ninapoangalia huu ukurasa, hasa nambari ya tano, naona wanaongea kuhusu madeni yaliyosalia. Tumeona hii serikali imekuwa na madeni yaliyosalia kila wakati, kila mwaka na kila mwezi na ni wananchi wamefanya hiyo kazi. Nafikiri hili ni jambo ambalo hiyo idara inafaa kuangalia, tusiwe na madeni yaliyosalia nyingi zaidi hadi waliotoa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

huduma kwa hiyo idara washindwe kufanya. Nimeona madeni yaliyosalia hapa zimekuwa milioni 144, ambayo ni pesa nyingi zaidi kwa robo ya kwanza.

Bwana Spika, mimi nakubaliana na kamati. Nimeona wana maoni yaliyo sawa. Nimeona wameweka mapendekezo ambazo nimezipitia na kuona kweli kamati wamefanya kazi yao na kuangalia jinsi ambavyo idara imetumia pesa. Nataka pia kumshukuru Mheshimiwa Wakahiu kwa kuisoma ripoti kwa njia ya urahisi ambapo kila mtu ameelewa, na amefanya hivyo kwa niaba ya Mheshimiwa Kanyutu ambaye yuko isipokuwa wakati huu mambo yamekuwa moto kule mashinani.

Ndipo naona tutakuwa tunaachia wengine wakati mwingine kwa sababu mtu akisikia kwake kuna moto kwanza anakimbia huko na kujaribu kuzima. Kwa hivyo, hawa Waheshimiwa wanakaa kama kila mtu ana zimamoto. Kukiwaka anakimbia kujaribu kuzima. Kwa hivyo tutafanya kazi tukiwa kitu kimoja ili tuweze kusaidiana kwa sababu hii ni kazi tunayofaa kusaidiana sisi sote bila kujali mtu ametoka kwenye kamati gani ama wapi. Tufanye kazi kama timu moja kwa vile hivi karibuni naona tukiachana na wengine, tutaachana kwa mwili bali roho zitakuwa pamoja.

Huenda wengine wakazama, na wakizama, kama nilivyosema juzi, wataenda kwa kazi zao. Watakaorudi watarudi kufanya kazi ya umma na watakaoenda wataenda kufanya kazi waliyokuwa wakifanya. Tulisema ni vizuri sisi sote tuwe tunakumbushana ya kwamba hapa si kwetu, sio majumbani kwetu. Tumekuja kazini hapa, unakuja leo bali kesho huenda ukafutwa. Kukiwa hivyo nafikiri sote tutafanya kazi kwa umoja.

Mimi nikiwa mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti leo, kukiwa na chochote kuhusu bajeti, naweza kutaka kuona hata Mheshimiwa Lochimidi akisimama hapa wima kuhakikisha kuwa bajeti imepita na kwamba mambo yote ya serikali inaendelea jinsi inavyostahili. Vilevile ningetaka kuona kama ni Idara ya Barabara, kama Mheshimiwa Jacob yuko pale na pengine mwenyekiti ama baadhi ya wanachama hawako, yeye anaingia hapo kwa sababu ana mamlaka ya kufanyia hiyo kamati kazi na anafanya kwa niaba ya hili Jumba.

Kwa hayo machache naunga mkono hiyo ripoti na tuweze kupitisha ilivyo maana huo ndiyo ukweli katika hiyo Idara. Ni idara ambayo tunafaa kuikodolea macho. Tuiangalie na pia tuchunguze yale mambo ambayo inaendelea. Nimesema pia Wajumbe ambao Wadi zao wananchi wao wanapewa maji na kampuni, waangalie hiyo maji kama ni safi ama imetibiwa na pia vile wanalipishwa. Kwa sababu kuna zile pesa wanastahili kulipishwa. Tujue mwananchi anaadhiriwa kwa njia gani. Tuko hapa kulinda mwananchi kwa njia yoyote ile. Kwa hayo machache, mungu awabariki na tuwe pamoja. Asante sana, Mheshimiwa Spika.

Hon. George Meshami: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Nashukuru kwa hii nafasi ya kuchangia ripoti ambaye imeletwa na Kamati ya maji na mali asilimu. Wacha niseme ya kwamba kamati wamejaribu kuleta ripoti ambayo ni sahihi. Kulingana na yale mapendekezo wamekuja nayo, wamesema ya kwamba kuna *pending bills* ambazo ni dhamana ya 144,601 ambaye zile *pending bills* hazijalipwa.

Angalau tunajua utekelezaji ya maji katika Kaunti yetu ya Laikipia imekuwa ikiendelea vizuri lakini *pending bills* ni yale madeni ambaye haijalipwa zile kampuni zimetunukiwa kazi ya kuchimba maji ama mabwawa. Ombi langu katika serikali wafanye juu chini walipe pesa kwa wenye kandarasi ambaye walitunukiwa kuendelea na kazi ya kufanyia kazi Wanalaikipia.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Pesa hizi zikiruka mwaka ujao, hawa wanakandarasi watakuwa na shida nyingi sana kuja kufuatilia pesa zao. Ombi langu ni kuhimiza serikali walipe zile pesa wakati unaofaa kabla ya mwisho wa mwaka huu ili Wanalaikipia waendelee kufaidika. Kuna mapendekezo pia wametaja ya kwamba kuna kazi ilifanyika ila haikumalizika.

Inafaa hiyo kazi ifuatiliwe na imalizwe kwa wakati unaofaa. Kulingana na Mjumbe wa Thingithu vile amesema, wakati huu vile tunaelewa ni wakati mgumu katika Kaunti yetu na nchi mzima. Kwa sababu tumekuwa na kiangazi kila mahali. Watu wameumia zaidi na hali ya maji hata mifugo wanaendelea kukufa kwa sababu ya hali ya kiangazi ambayo imetanda nchi mzima.

Ila yangu ni kuomba Serikali wapate kusukuma mashine za kusambaza maji mahali ambapo kuna kiu ya maji. Kuna sehemu kama ile Wadi yangu ambayo nawakilisha, kuna mahali panaitwa Musul, Motiok na Ewaso Nyiro ambayo maji yamekatika.

Sasa hakuna maji ambayo inatembea na ukipata maji, unapata maji ambayo imesimama na imechafuka zaidi. Ningependa Serikali wapate kutilia mkazo na wapate kuletea watu maji. Asante sana, pia nami naunga hii ripoti mkono.

Speaker: May I ask the mover to give a reply.

Hon. Wilson Wakahiu: Thank you, I want to appreciate the contribution of the Hon. Members who have also talked of what the department has done. I want to concur with my Hon. Members who have already spoken concerning how the department and even how the situation is, as far as pending bills are concerned and also the situation that we are in now. That is the issue of this period when we have no water in our rivers as well as the supply in our towns.

Mr. Speaker, this department as far as pending bills are concerned is one of the departments that receives conditional grants from donors and at some time they did not receive in time hence they were unable to may be do any project because they were waiting to be funded by donors. The issue of having maybe the low supply have been done because of having not received funds from the conditional grants.

I want to thank Hon. Meshami and Hon. Kagondu because of their contribution and we have to understand that, now we are suffering because of shortage of water. Given the drought that our county and the country is experiencing right now. Even in my place Salama, people are not getting water even for domestic use.

Now as they have said, we need to work together irrespective of which committee you are in to ensure our people do not suffer or the livestock. I want to appreciate the contribution of Members, those who have spoken and also those who also support this report. Thank you.

(Question put and agreed to)

Speaker: I just want to inform Members that some of us are not here because they are attending the EALASCA games. You know we have East Africa games that are happening in Eldoret. Last year they were in Kampala, Uganda, this year they are in Eldoret, Kenya. Therefore, the committee that is in charge of sports, Labour, and also our two teams, that is Badminton and Ajua are attending and participating. It is important because they are the ones left behind that we also represent them well here making sure that initially we have Quorum as we continue participating with the business of the House.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ADJOURNMENT

Speaker: This House stands adjourned until tomorrow, Wednesday 9th March, 2022 at 9.00 a.m.

The House rose at 2.52 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*